

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 022 2126826
Nukushi: 022 2126834
Tovuti: www.habari.go.tz
Baruapepe: km@habari.go.tz



Mji wa Serikali
Mtaa Wa Habari,
S. L. P. 25,
Mtumba,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb) ametuma salamu za pole kwa familia ya aliyekuwa Mhariri wa Habari wa Gazeti la Jamhuri Bw. Godfrey Dilunga ambaye amefariki jana jijini Dar es Salaam.

Dkt. Mwakyembe ameeleza kuwa kifo cha Bw. Dilunga ni pigo kwa tasnia ya Habari na michezo pia kwa kuwa enzi za uhai wake alikuwa ni mmoja wa wanakamati wa Masoko na Habari katika Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF).

“Kwa Hakika tumepoteza mtu muhimu sana katika tasnia yetu ya habari pamoja na michezo , Mungu awape nguvu wanafamilia wote” amesema Dkt. Mwakyembe.

Enzi za uhai wake Bw. Dilunga amewahi kufanyia kazi katika magazeti ya Raia Mwema na Mtanzania akiwa mmoja wa Wahariri wa vyombo hivyo vya habari.

Dkt. Mwakyembe ametoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki pamoja na tasnia ya habari kwa kuondokewa na mpendwa wao.

Imetolewa na:-

Lorietha Laurence
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.
18/09/2019